**Masomo ya Watoto**

# Kutafuta Hazina Katika Neno la Mungu

*Masomo ya Juma*

*La Maombi*

*3 – 10 November 2018*

Masomo haya yametayarishwa na
Idara ya Huduma za Familia
Halmashauri Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato
Kwa kushirikiana na Idara ya Huduma za Familia
Union ya Kaskazini mwa Tanzania (NTUC)
Yametafsriwa na Moseti Chacha

## Yaliyomo

Utangulizi

Kutafuta Hazina katika Neno la Mungu ….…………………………………...………. 2

**Sabato ya Kwanza 3 Novemba 2017**

Kwa Nini Tunathamini Biblia? …………...…………………….………………….………… 3

**Siku ya Jumapili 4 Novemba 2017**

Soma Biblia – Inaweza Kuaminiwa? ………………...……….……………...…...……… 5

**Siku ya Jumatatu 5 Novemba 2017**

Chunguza Biblia – Namna Ninavyosoma Biblia ….…………………...……………. 7

**Siku ya Jumanne 6 Novemba 2017**

Kutumia Hazina ya Mungu – Biblia Inaniongoza ……….……………………….………. 9

**Siku ya Jumatano 7 Novemba 2017**

Biblia Inanionyesha Yesu ………………………..……..…………………………....… 10

**Siku ya Alhamisi 8 Novemba 2017**

Kuelewa Hazina ya Tumaini …………………...…….……………………..……..…. 13

**Siku ya Ijumaa 9 Novemba 2017**

Sahihi na Isiyo Sahihi – Biblia Inanisaidia Kuona Tofauti………...…………………… 15

**Sabato ya Pili 10 Novemba 2017**

Kutiwa Moyo na Biblia……………………………………………………………..…... 17

# Utangulizi

## KUTAFUTA HAZINA KATIKA NENO LA MUNGU

*Julie Weslake alikuwa mwalimu na mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Watoto wa Divisheni ya Kusini mwa Pasifiki. Ana shauku kuhusu makanisa na familia kujenga imani ya watoto.*

Biblia ni kama ramani ya hazina. Kadri tutakavyosoma Biblia kwa pamoja juma hili tutatafuta mafungu ambayo hutufundisha kuhusu:

- Hazina katika Biblia
- Kuitegemea Biblia
- Kuchunguza maneno
- Kuifanyia kazi Biblia
- Kumuona Yesu
- Kuelewa tumaini
- Ukweli na uongo
- Kutiwa moyo

**Kwa waalimu wa Watoto:**

Mwisho wa kila somo la siku kuna kipengele cha "Hebu tutengeneze." Kipengele hiki kinahitaji vifaa vya kutumia ili watoto wajihusishe kutengeneza kama inavyoelekezwa. Ni vema mwalimu akatayarisha vifaa vinavyohitajika kukamilisha kile kinachotakiwa kutengenezwa mapema kabla ya somo. Pengine siku moja kabla.

Vifaa vitakavyotayarishwa vinatakiwa viwe vingi vya kutosha kulingana na idadi ya watoto alio nao mwalimu katika darasa ili kila mtoto ashiriki kutengeneza mwenyewe.

SABATO YA KWANZA

# Kwa nini Tunathamini Biblia

**Fungu Elekezi:** "Bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako" Mathayo 6:20, 21.

Gemma alikuwa ametengeneza boksi dogo la pekee na kulipamba kwa picha. Alitaka kumpatia Bibi yake, kwa sababu alimpenda sana Bibi yake. Gemma alifahamu mahali hasa ambapo angeliweka hilo boksi. Aligundua sehemu ambayo Bibi yake anaweka hazina zake, hivyo aliliweka kwa umakini kwenye kabati pembeni ya mapambo na picha zake ambazo huyo Bibi alipenda kuziangalia.

Kwenye kabati kulikuwa na kitabu. Gemma aliwaza kwamba kitabu hiki kitakuwa cha pekee kwa sababu kilikuwa kwenye kabati la pekee. Lakini alipofungua kurasa za kitabu kile alishangaa sana kwa sababu kuna mtu alikuwa ameandika ndani ya kitabu hicho na kupigia mstari baadhi ya aya na maneno. Gemma alifahamu kwamba kamwe haupaswi kuandika au kuchora ndani ya vitabu, hivyo alimuuliza Bibi yake kuwa kwa nini kitabu chake cha pekee kilikuwa kimepigiwa mistari na kuandikwa andikwa.

Bibi alieleza kwamba kitabu kile kwa hakika kilikuwa cha pekee. Kiliitwa Biblia. Bibi alisema kwamba alikuwa akikisoma kila siku. Maneno yaliyoko ndani yake, hasa yaliyopigiwa mistari, yalikuwa hazina alizotaka kukumbuka kwa sababu zilimuunganisha na Yesu kwa upendo wake kwake. Bibi alisema kwamba maneno yale yalimwonyesha jinsi ya kumpenda Yesu na namna ya kuwa kama yeye. Jumbe hizo zilimpatia kusudi la kila siku na tumaini la siku zake zijazo. Bibi alisema kwamba asingeweza kuishi bila kusoma jumbe alizopatiwa na Mungu kila siku.

Gemma alifurahi sana. Alitaka pia kumpenda Yesu na kufahamu kumhusu yeye zaidi. Alitaka maneno ya hazina ili yafanye maisha yake kuwa yenye furaha zaidi. Hivyo alimuomba Bibi amuonyeshe namna ya kusoma na kuielewa Biblia na kuishi na Yesu kama rafiki yake wa karibu.

Bibi alifurahi sana. Alisema kwamba hakukuwa na cho chote cha muhimu Zaidi ya kushiriki maneno yaliyoko ndani ya Biblia. Alielezea kwamba Biblia ilikuwa kama kuwa na ramani ya hazina, na kwamba unapotumia muda kuisoma Biblia, ni kama kuchimba ukitafuta dhahabu, fedha, au vito vya thamani.

Katika kitabu cha Mathayo sura ya 6, Yesu anatusihi tusiishi tukijaribu kutafuta hazina za hapa duniani. Badala yake tunapaswa kutumia muda na mali kwa vitu

ambavyo Yesu angependa tutumie, ili kwamba hazina zetu ziwe mbinguni. Kwa sababu zilipo hazina zetu, ndipo na mioyo yetu ilipo. Hebu tusome hayo mafungu:

> "Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako." (Mathayo 6:19-21)

Tukisoma hadithi inayopatikana katika Mathayo 13:44-46 Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba mbingu ni kama hazina katika shamba. Unaweza kutaka kuuza vyote ulivyo navyo ununue shamba lile ili uweze kuipata hazina hiyo. Furaha ya kuwa na Yesu mbinguni na kuishi pamoja naye milele ni ya thamani sana kama hazina hiyo. Ili tuweze kufika mbinguni, tutafurahi kuacha mambo mengi katika maisha yetu na kutumia muda wetu kusoma Biblia.

**Hebu Tuzungumze**

Ni jambo gani la thamani unaloweza kutumia muda na mali yako ili uweze kupokea hazina zinazopatikana katika Biblia?

---

---

**Tuombe**

Mwombe yesu akusaidie kutafuta hazina za muhimu katika Neno lake (Biblia) ambazo unahitaji ili kuishi maisha matakatifu. Mshukuru kwa hazina ambazo amekwisha kupatia.

**Hebu Tutengeneze**

Chora ramani ya hazina ya chumbani kwako, kanisani, au nyumbani. Ficha mafungu ya Biblia na onyesha kwenye ramani ya hazina namna ya kupata mafungu hayo. Marafiki au familia yako wanapopata mafungu hayo, muyasome pamoja.

JUMAPILI

# Soma Biblia – Inaweza Kuaminiwa

**Fungu Elekezi:** "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema" (2 Timotheo 3:15, 16).

Bibi alimwonyesha Gemma sehemu inayosema kwamba Biblia ni kitabu cha Mungu. Kinaitwa Maandiko Matakatifu kwa sababu hutuambia kuhusu Mungu na namna ya kumpatia mioyo yetu na kuishi kwa ajili yake. Bibi alielezea kwamba kwa hakika Biblia haikuwa kitabu kimoja, lakini ni vitabu vidogo 66 – vilivyoandikwa na watu tofauti, baada ya Mungu kuwapatia mawazo na maneno. Watu waliandika kile walichokumbuka kuhusu jambo lililotokea muda mrefu uliopita, na baadhi waliandika kuhusu kipindi Yesu alipokuwa duniani. Baadhi waliandika nyimbo au mashairi, na baadhi waliandika vitu ambavyo vinatazamiwa kutokea siku za mbele.

Biblia inatuambia kwamba jumbe zilizo ndani ya Biblia hazikutoka mawazoni mwa waandishi tu. "Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu" (2 Petro 1:21).

Kitabu kimoja katika Biblia hutuambia kuhusu mvulana mmoja aliyeitwa Timotheo ambaye alipata hazina ya Biblia. Aliigundua Biblia kupitia kwa mama yake aliyeitwa Eunike, na bibi yake aliyeitwa Lois. Walifahamu ni kwa namna gani maneno ya Biblia yalivyo ya thamani, na hivyo waliamua kwamba ni muhimu kukaa na Timotheo kila siku na kumfundisha namna ya "kuchimba ili kutafuta hazina" katika Biblia na kumpatia Yesu moyo wake.

Kwa sababu Biblia ilivuviwa na Mungu, Timotheo alijenga imani kwa Yesu iliyompatia ujasiri na shauku ya kushiriki na wengine habari za Yesu na kuwaongoza watu kuishi kwa ajili yake.

Watu wa Thesalonike waliamini pale Sila na Timotheo walipowaambia kuhusu hazina ya Biblia na wakageuka kutoka kwenye kupenda sanamu na wakaanza kumpenda Yesu, ambaye ni Mungu aliye hai. Paulo alimsifu Mungu kwa jambo hili. Aliwaandikia Wathesalonike akisema, "Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa, mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini" (1 Wathesalonike 2:13).

Bibi alimuuliza Gemma kama alifahamu imani ni nini. Gemma alisema Imani ilikuwa kama kuamini kwamba Baba atakudaka pale anapokuambia uruke kwenye bwawa la kuogelea.

Bibi alisema kwamba kusoma Biblia, na kuamini kwamba maneno yake yalitoka kwa Mungu; na kutenda kile kinachosemwa ilikuwa ni kama kusoma na kufuata maelekezo ya mapishi na kuamini kwamba ulichoandaa kitaiva na kuwa keki.

**Hebu Tuzungumze**

Ni vitabu na programu zipi ambazo umesoma au kuangalia ambazo unafahamu kwamba si halisi? Ni vitabu au programu gani ulizo nazo ambazo ni halisi na za kweli?

**Tuombe**

Mwombe Mungu akusaidie kuweka umakini wako kwenye hadithi za Biblia ambazo ni halisi na zinaweza kukusaidia kukua, badala ya hadithi zisizo za kweli na ambazo ni maburudisho tu.

**Hebu Tutengeneze**

Panga viti katika chumba kwa mfumo wa kizuizi. Andika maelekezo ya mtu kusoma atakapokuwa akimsidia mtu mwingine aliyefunikwa macho kwa kitambaa ili aweze kupita kizuizi hicho. Kwa mfano, andika ni hatua ngapi kushoto, kulia au mbele, ambazo anahitaji kutembea ili aweze kutoka salama.

JUMATATU

# Chunguza Biblia – Namna Ninavyosoma Biblia

**Fungu Elekezi:** "Vivyo hivyo haipendezi mbele za Baba yenu aliye mbinguni kwamba mmoja wa wadogo hawa apotee" Mathayo 18:14.

Gemma alimwambia Bibi yake kuhusu wakati alipokuwa na mama yake wakichunguza bustani mpya ya wanyama na kwamba hawakuweza kupata sehemu walipohifadhiwa ndege. Iliwabidi kusimama na kutazama ramani ya bustani ile ili iwapatie maelekezo ya kuelekea njia sahihi. Ilikuwa inachekesha kwa sababu walikuwa wakizunguka tu wakati sehemu walipohifadhiwa ndege ilikuwa na umbali wa mwendo wa dakika tano tu.

Bibi yake alicheka na akasema jambo hilo linafanana na baadhi ya watu wanaojaribu kumtafuta Mungu na kusudi lake na furaha ya maisha yao. Nyakati zingine wanatazama kila mahali na kujaribu vitu vingi, lakini kumbe Mungu yupo karibu sana. Wanahitaji tu kusoma Biblia zao. Watu wengi wanafikiri kwamba Biblia ni ngumu sana kusoma, kwamba ina mambo mengi sana. Wakati mwingine hawaamini kwamba Biblia kwa hakika ni Maneno ya Mungu kwao. Nyakati zingine wanafikiri Biblia imejawa tu na sheria.

Namna iliyo bora ya kuanza kuchunguza Biblia ni kuomba kwanza. Roho Mtakatifu wa Mungu hutusaidia kuelewa tunachokisoma. Yesu aliporudi mbinguni, aliahidi kwamba angetuma "Roho wa kweli" ili awe pamoja nasi milele. "Huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote" (Yohana 14:17, 26).

*Mpendwa yesu, tafadhali nisaidie leo kuelewa ninachokisoma katika Biblia ambayo ni Neno Lako.*

Bibi alimwambia Gemma kwamba alitamani angempatia miwani ya pekee ya kusomea Biblia, ili kwamba anapoivaa miwani hiyo aone Mungu ni nani na anafananaje. Kama miwani kama hiyo ingekuwepo, ingetuonyesha kwamba jambo la muhimu sana kumhusu Mungu ni kwamba anatupenda. Tunapochunguza maneno mengi ndani ya Biblia, tunahitaji kuvaa miwani yetu ya "Mungu ni upendo." Ni rahisi kuona upendo wa Mungu katika mafungu haya: "Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake" (1 Yohana 4:16). "Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza" (1 Yohana 4:19).

Ujumbe mkuu wa upendo katika Biblia kumhusu Mungu ni kwamba alimtuma Mwana wake Yesu, ili afe kwa ajili yetu: "Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea" (Luka 19:10).

Mungu anatupenda sana kiasi kwamba atatutafuta kama mchungaji amtafutavyo mwanakondoo aliyetanga mbali, akapotea, na hawezi kurudi nyumbani. Mungu ni ramani ya hazina, tena yeye ndiyo hazina yenyewe.

*Mpendwa Yesu, tunakushukuru kwa kutupenda, licha ya kwamba hatustahili. Tusaidie kuona upendo wako katika kila tunachosoma ndani ya Biblia.*

**Hebu Tuzungumze**

Ni njia gani nyingine tofauti na kusoma, unayoweza kutumia ili kupokea ujumbe wa Biblia?

---

---

**Tuombe**

Mwombe Mungu ashiriki mpango wake kwa maisha yako kadri unavyojifunza neno lake kwa uaminifu.

**Hebu Tutengeneze**

Buni na utengeneze baadhi ya "miwani ya Mungu ni upendo" kwa ajili ya usomaji wa Biblia. Unaweza kutengeneza kwa kutumia mbao nyembamba na plastiki au karatasi ya plastiki. Au unaweza kutengeneza kwa kukunja vijaa vya kusafishia mirija.

JUMANNE

## Kutumia Hazina ya Mungu – Biblia Inaniongoza

**Fungu Elekezi:** "Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote." (Yohana 15:5)

Gemma alipenda kuwatengenezea watu vitu mbali mbali hata kusaidia nyumbani na shuleni. Lakini wakati mwingine hakujisikia kusaidia, na wakati mwingine alihisi amekosea kuchagua hasa watu walipomkasirisha au kumhuzunisha. Anasema kuwa mara nyingi alijaribu kadiri alivyoweza, lakini hakuona mabadiliko. Alikuwa akishangaa hazina zilizopo katika Biblia na kujiuliza kama zingeweza kumsaidia kuwapenda watu zaidi na kumsaidia kufanya maamuzi sahihi.

Bibi alimhakikishia kwamba watu wote hufanya makosa, na kwamba hazina tunazosoma katika Biblia zinaweza kutusaidia. Hazina ya kwanza ya Biblia tunayopaswa kukumbuka ni kuwa, hata kama hatuoni tofauti, bado tunatakiwa kuendelea kusoma Biblia. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba hazina hii inafanya kazi kama mzabibu: tawi (yaani sisi) likiendelea kuwa ndani ya mzabibu (yaani Yesu), mzabibu utaendelea kuzaa zabibu. (Yohana 15:5). Kwa hiyo tunatakiwa kila siku tuwe tumeunganika na Yesu kupitia katika kusoma Biblia. Muunganiko huu unatusaidia kutenda na kuenenda kama Yesu kwa kufanya maamuzi yaliyo sahihi kila siku. Mzabibu unapozaa matunda, wengine nao watayafurahia pia. Tunapozaa matunda ya hazina ya Bibila, tunaweza kuwabariki wengine pia.

Kama hadithi aliyoikumbuka Gemma kutoka kwenye Biblia kumhusu binti mdogo wa Kiisraeli aliyekuwa mtumwa ambaye alimwambia bwana wake alipokuwa mgonjwa kuhusu nguvu ya uponyaji ya Mungu. Kwa sababu alijali na kushiriki maarifa aliyokuwa nayo kumhusu Mungu ambayo aliyapata kutoka kwenye hazina za Biblia, bwana wake, jemedari Naamani, aliponywa. Unaweza kusoma hadithi hii katika 2 Wafalme 5:1-14.

Bibi alielezea kwamba mambo yote mema tunayofanya hutoka kwa Yesu, na kwamba tunapaswa kumshukuru kwa kutusaidia. "Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo, tunazofarijiwa na Mungu" (2 Wakorintho 1:3, 4).

Gemma alitaka sana kuwa kama Yesu. Bibi alielezea kwamba inachukua muda wa maisha yote kuwa kama Yeye, na ni kwa kupitia katika kusomba Biblia na kuomba kila siku tu ndipo tunakua taratibu: "Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na

mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho" (2 Wakorintho 3:18).

Dumu kuunganika na Yesu kupitia katika kusoma neno lake naye atakupatia moyo wake, sauti yake, mikono yake na miguu yake ili uweze kushiriki upendo wake na wengine.

**Hebu Tuzungumze**

Kama ungetumia muda wa siku nzima na Yesu, ungependa kuzungumza naye kuhusu nini? Ungependa mwende wapi? Mngefanya nini?

---

---

**Tuombe**

Mwombe Yesu amtume mtu leo ambaye utaweza kushiriki naye baadhi ya maneno ya hazina uliyoyagundua katika Biblia.

**Hebu Tutengeneze**

Jifunze mzunguko wa maisha ya kipepeo au chura. Tambua mabadiliko makubwa yanayofanywa na nguvu ya Mungu. Sisi pia tuna nguvu hii ya kubadilisha tunapoiomba na kuunganishwa kwa Yesu kupitia kwenye Biblia.

JUMATANO

# Biblia Inanionyesha Yesu

**Fungu:** "Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao" Mathayo 1:21.

Inafurahisha kugundua kuwa ni kwa nini tulipewa majina yetu na yanamaanisha nini.

Gemma alifurahi kugundua kwamba jina lake kwa Kifaransa linamaanisha "kitu cha thamani," na kwa Kingereza linamanisha "jiwe la thamani." Mwana wa Mungu alipotakiwa kuzaliwa, malaika wa Bwana alimtokea baba yake wa duniani, Yusufu, na kumwambia kwamba alipaswa kumpatia jina "Yesu." Ni jina maalum lililochaguliwa na Mungu kwa sababu humaanisha kwamba atakuwa Mwokozi wa ulimwengu.

Biblia inatumia majina mengi kumtaja Yesu, na yote hudhihirisha kuwa yeye ni nani, tabia yake, na utume wake. Bibi alimuomba Gemma aende kumletea Biblia, ili waweze kuchunguza mafungu na kutafuta majina tofauti ya Yesu. Waliandika majina yote kwenye karatasi kubwa. Hapa kuna baadhi ya majina hayo:

***Imanueli***, Mathayo 1:23: "'Tazama, bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake **Imanueli**'; Yaani, 'Mungu pamoja nasi'." Mungu hakutaka kuwa Mungu wa mbali, alitaka kuishi kati yetu. Yesu alikuwa Mungu duniani.

***Mwana wa Mungu***, Yohana 3:16: "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Kwenye ubatizo wa Yesu, Mungu alimthibitisha kama Mwana Wake. "Na sauti ikatoka mbinguni, 'Wewe ndiwe **Mwanangu**, mpendwa wangu; nimependezwa nawe'" (Marko 1:11)

***Mwana wa Adamu***, Marko 10:45: "Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi," Yesu pia anaitwa ***Mwana wa Adamu***. Yesu alikuwa Mungu lakini alizaliwa na mama wa kidunia, Mariamu. Kitendo hicho kinamfanya Yesu kuwa wa pekee sana kwa sababu alikuwa Mwana wa asili ya kibinadamu, na pia alikuwa Mwana wa Mungu.

***Neno la Mungu***, Yohana 1:1, 14: "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Yesu alimdhihirisha Mungu kwetu. Ndiye alikuwa Neno la Mungu. Hapo mwanzo, alitamka na ulimwengu ukawa! "Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi" (Wakolosai 1:15, 16). Yesu

hakuivuvia Biblia tu, ambayo ndilo Neno la Mungu kwetu, lakini Yesu *ndiye* Neno la Mungu. Tukimfahamu yeye, tumemfahamu Mungu.

Kuna majina mengine mengi ya Yesu ndani ya Biblia. Waombe wazazi au waalimu wako kukusaidia kugundua baadhi ya majina hayo. Hapa kuna baadhi ya sehemu unazoweza kuanzia:

Mwanakondoo wa Mungu: Yohana 1:29, 36

Alpha na Omega: Ufunuo 22:13

Mkate wa Uzima: Yohana 6:35

**Hebu Tuzungumze**

Tafuta maana ya jina lako, na kwa nini ulipewa jina hilo.

---

**Tuombe**

Mwombe Yesu akusaidie kuelewa maana ya thamani ya majina yake yote kadri unavyojifunza Neno la Mungu.

**Hebu Tutengeneze**

Andika majina ya Yesu kwenye vipande vya karatasi ambavyo vinafanana urefu. Tengeneza mnyororo wa karatasi na utundike katikati ya picha ya Yesu na picha yako pamoja na familia yako.

ALHAMISI

## Kuelewa Hazina ya Tumaini

**Fungu Elekezi:** "Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini" Warumi 15:4.

Gemma alipenda shule, lakini daima alikuwa akisubiri kwa hamu wakati wa likizo. Mwaka huu wangekwenda kumsalimia Bibi. Mama alikata tiketi miezi michache kabla ya safari, na kwa Gemma wakati wa likizo ulionekana kuchelewa sana. Alimwambia Bibi jambo hili katika maongezi kupitia simu.

Bibi alijaribu kumtia moyo Gemma. Alimuelezea kwamba kusubiri kwa hamu kitu kunafahamika kama kuwa na tumaini. Unapanga kwa ajili ya jambo hilo, unakata tiketi, na kuweka nguo zako tayari. Bibi pia alitamani wakati wa likizo ufike. Bibi aliahidi kumkumbatia Gemma watakapokutana uwanja wa ndege.

Bibi na Gemma waliongea kuhusu tumaini ambalo Biblia hutoa. Kwa sababu Adamu na Hawa waliamua kumsikiliza Shetani, Warumi 1:25 inatuambia kwamba watu walianza kuabudu na kutumikia vitu vilivyoumbwa badala ya Mungu kama Muumbaji. Watu walianza kufanya mambo mengi yaliyokuwa maovu na ya kuumiza, na kutotumia muda kujifunza kumhusu Mungu na kumuamini. Lakini kwa sababu Mungu anatupenda sana, alifanya mpango wa kuwaokoa wale ambao wangemgeukia. Mpango wa Mungu ungemzuia Shetani pamoja na dhambi kuwaumiza watu wake. Mwana wa Mungu, Yesu, angekuja duniani kama mtoto. Ingawa Yesu hakuwahi kufanya kosa lo lote, angekufa kwa ajili ya dhambi zetu, ili tuweze kusamehewa na kuishi na Yesu milele mbinguni. Upendo wa Mungu hutupatia tumaini kwamba tutakwenda mbinguni na tutaweza kuishi pamoja naye milele. Bibi alishiriki fungu la hazina pamoja na Gemma wakati Yesu aliposema:

"Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo" (Yohana 14:1-3).

Kadri Gemma alivyofikiria likizo, alifikiria itakavyopendeza Yesu atakapokuja. Kisha yeye pamoja na Bibi watakuwa pamoja na Yesu milele. Ghafla Gemma alijawa na shauku sana ya kuja kwa Yesu. Alimpigia simu Bibi na kumueleza. Bibi alifurahi sana kusikia kwamba Gemma alikuwa na shauku ya kuja kwa Yesu. "Tuna tumaini zuri sana, Gemma," alisema Bibi. "Ni tumaini linaloufanya moyo wangu uimbe. Ni tumaini kwamba siku moja Yesu ataonekana angani, na atawaamsha hata wafu waliompenda."

"Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele" (1 Wathesalonike 4:17).

Gemma alisema alitamani sana! Je, wewe unatamani?

**Hebu Tuzungumze**

Ni kwa namna gani unaweza kuelezea tumaini kwa mvulana au msichana mwenzako?

**Tuombe**

Mwombe Yesu akusaidie ili umpatie moyo wako kila siku, hatimaye uende naye mbinguni siku atakapokuja.

**Hebu Tutengeneze**

Tengeneza boksi la ahadi. Tengeneza boksi dogo na lipambe kwa michoro na picha. Kata vipande vidogo vya karatasi vyenye ukubwa unaofanana na andika mafungu yako ya tumaini unayoyapenda zaidi. Kunja vipande hivyo vya karatasi na uviweke katika boksi hadi litakapojaa. Soma fungu moja kila siku, au mpatie rafiki boksi hilo la ahadi.

IJUMAA

## Sahihi na Isiyo Sahihi – Biblia Inanisaidia Kuona Tofauti

**Fungu Elekezi:** "Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote.' … 'Mpende jirani yako kama nafsi yako'" (Marko 12:30, 31).

Bibi aliona kuwa Gemma alikuwa na wasiwasi. Alikuwa amemsikia akigombana wakati akicheza na kaka yake asubuhi ile. Maneno ya hasira yalikuwa yamenenwa. Mama alipomwambia aombe msamaha, Gemma alichagua kunyamaza kufunga mdomo wake kwa nguvu ili maneno yo yote yasitoke. Sasa Gemma alikuwa ameketi nje kwenye ngazi akionekana kuwa na huzuni.

Bibi alifahamu kwamba kulikuwa na mafungu mengi ya hazina kutoka kwenye Biblia ambayo yangemsaidia Gemma kuchagua kufanya jambo lililo sahihi. Alimkumbusha Gemma kuweka miwani yake ya "Mungu ni upendo." Kisha walifungua Biblia ya Bibi na kuanza kusoma na kuzungumza.

Katika Marko 12 Yesu alisema kwamba amri iliyo kuu ilikuwa kumpenda Mungu kwa moyo wote, muda wote, na nguvu zote tulizo nazo; na kwamba ya amri ya pili iliyo kuu ilikuwa kumpenda jirani kama nafsi yetu. Bibi alielezea kwamba tunapokuwa hatuna uhakika wa jambo la kufanya, tunapaswa kufikiri, *Ninajiuliza kuwa Je, ninaweza kumpenda Mungu na jirani yangu kwa namna gani iliyo bora?* "Gemma," alisema Bibi, "Nina uhakika kwamba Yesu anamchukulia kaka yako na watu wote katika maisha yako, hata mtaani kwako na zaidi, kama jirani yako."

"Kama unampenda kaka yako, utajaribu kumwambia maneno mazuri. Tunapoanza kuhisi hasira tunaweza kuondoka na kutembea mbali hadi tutakapohisi tumetulia. Kama tunataka kuishi na mama kwa upendo wa Yesu, tunapaswa kumtii. Katika Mithali 15:1 tunasoma, "Jawabu la upole hugeuza hasira; Bali neno liumizalo huchochea ghadhabu."

Gemma alifikiria kwa muda na kisha alitoka kwenda kumtafuta Mama. Alitaka kumuomba msamaha.

Kwanza Yohana 2:3-8 inatuambia kwamba tunamfahamu Yesu ikiwa tunatii amri zake, tunatii neno lake na kuenenda kama alivyoenenda. Baadhi ya maagizo ya muhimu kutoka kwa Mungu walipatiwa wana wa Israeli na hata sisi, kupitia kwa Musa. Yesu aliishi akifuata Amri hizi Kumi. Nne za kwanza hutuambia namna ya kumpenda Mungu na sita zinazofuata hutuambia namna ya kupendana. Bibi alimsomea Gemma Amri Kumi katika Kutoka 20 na kumuelezea.

Bibi alisema, “Gemma, kila mmoja anafanya makosa. Lakini sote tunaweza kuomba Mungu atusamehe, na kufanya kazi kwa bidii katika kudumu tukiwa tumeunganishwa kwa Yesu. Yesu aliahidi kwamba siku moja tutaishi na kupenda kama yeye. Kwanza fungu la Yohana 3:2 linatuambia kwamba atakapodhihirishwa tutafanana naye, kwani tutamuona kama alivyo. “Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu” (Wakolosai 3:12).

**Hebu Tuzungumze**

Mwongozo mzuri wa kuchagua lililo sahihi na lisilo sahihi ni upi?

---

**Tuombe**

Mwombe Yesu atusaidie kuomba msamaha kwa wengine tunapokuwa tumekosea.

**Hebu Tutengeneze**

Tengeneza boksi la nguo. Weka alama katika kila nguo kwa kitendo au tabia. Baadhi zitawekwa alama kwa maneno kama: upole, kushiriki, kusoma Biblia, kuomba, na zingine zitawekwa alama kwa maneno kama: kucheza michezo ya video, kuwa mbinafsi, kudanganya, na kuiba. Chagua nguo na ziweke kwenye boksi, tunaweka nguo katika begi kwa ajili ya mbinguni.

SABATO YA PILI

# Kutiwa Moyo na Biblia

**Fungu Elekezi:** "Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu … Shuhuda zako nimezifanya urithi wa milele, Maana ndizo changamko la moyo wangu" Zaburi 119:105-111.

Muda wa Gemma kufungasha mabegi yake na kurudi nyumbani ulikuwa umekaribia. Alifurahia kutumia muda wake na Bibi yake akipata hazina katika Biblia. Atakumbuka sana kuzungumza na Bibi. Bibi yake alimkumbusha kwamba hazina walizopata sasa zilikuwa mioyoni mwao, hivyo Gemma angeenda nazo nyumbani. Gemma alikuwa na Biblia yake mwenyewe na alifahamu kwamba Mama na Baba wangemsaidia kutafuta hazina zaidi.

Tunapohisi kupotea kidogo na kutokuwa na uhakika wa namna ya kudumu kuuunganika na Yesu, tunaweza kuamini Neno la Mungu. Biblia ni kama mwanga au tochi ya kuonyesha namna ya kudumu kuishi kwa namna anayotaka Yesu.

Bibi alielezea kwamba ulimwengu huu si makazi yetu ya kudumu. Tunatazamia kwenda nyumbani mbinguni. Hata hivyo, muda huu unavyozidi kukaribia, watu watakataa kumpenda Mungu na kumfuata Yesu. Bila hazina za Biblia ndani ya mioyo yao watapata shida jinsi ya kuwa wema kwa wenzao na kusaidiana. Ulimwengu utakuwa sehemu ngumu sana ya kuishi.

Yesu alisema kwamba yeye ni "nuru," na kwamba yeye ni "njia, na kweli, na uzima" (Yohana 14:6). Kuunganishwa na Yesu kupitia katika usomaji wa Biblia na maombi kutadumisha na kuimarisha upendo wetu kwa Yesu. Mathayo 6:33 inatuambia "utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake, na hayo yo te mtazidishiwa."

Gemma alikumbuka hadithi kumhusu mtu mwenye hekima aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba, na mtu mpumbavu aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga. Mafuriko yalipokuja, nyumba iliyokuwa juu ya mwamba tu ndiyo iliyosimama imara. Yesu alisema kwamba mtu mwenye hekima aliyasikia maneno yake na kuyafanyia kazi. Watu wengi husikia kumhusu Yesu na upendo wake, lakini si wengi wanaoukubali upendo huu na kumpenda Yesu kiasi cha kutosha kumwamini na kuishi kwa ajili yake.

Bibi alimwambia Gemma kwamba Yesu alimtaka ashiriki upendo wake na kuwafanyia watu wengine mambo mema: "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni" (Mathayo 5:16). Inafurahisha sana kuwa nuru ya Mungu na tumaini la watu.

"Hivyo mfuateni Mungu, kama watoto wanaopendwa; mkaenende katika upendo, kama Kristo naye alivyowapenda ninyi tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato" (Waefeso 5:1-2).

**Hebu Tuzungumze**

Ni hazina gani nane tulizojifunza juma hili?

---

---

**Tuombe**

Mwombe Yesu akupatie uelewa wa kina wa upendo wake kwetu.

**Hebu Tutengeneze**

Tengeneza kitenganishio cha Biblia. Andika juu yake fungu la hazina ambalo unalipenda sana katika juma hili. Lipambe kwa picha. Funga kitambaa kidogo kizuri ili kining'inie kwenye ukurasa wa Biblia unaousoma.